

### Taarifa kwa Vyombo vya Habari

#### **Operesheni ya Kishujaa ya Wanajihadi Hossam na Amer Dhidi ya Wanajeshi wa Kiyahudi Inakanusha Udhuru Wowote kwa Jeshi Kushindwa Kuchukua Hatua dhidi ya Umbile lao (Imetafsiriwa)**

Operesheni ya kishujaa, ambapo vijana wawili kutoka Jordan, Amer Al-Qawas na Hossam Abu Ghazaleh, waliuawa shahidi walipokuwa wakipenya kwenye mipaka ya Palestina inayokaliwa kimabavu kusini mwa Bahari ya 'Dead Sea' kwa miguu na kuwashambulia kwa ujasiri wanajeshi wa Kiyahudi, na kusababisha majeraha na pengine vifo, inabeba athari kubwa ambazo lazima zizungumziwe. Inahitajika pia kuzungumzia misimamo ya wale ambao wameshindwa kupongeza operesheni hii:

- Umma, ukiwa umefungwa minyororo ya tawala za kihaini zinazoshirikiana na umbile la Kiyahudi, haujanyamaza na hautakaa kimya mbele ya vitendo vya kikatili vya mauaji ya halaiki vinavyofanywa na umbile la Kiyahudi dhidi ya watu wa Palestina na Lebanon, na hata Jordan. Jordan, iliyomtoa shahidi Maher Al-Jazi, itaendelea kutoa mashahidi mashujaa (shuhadaa) ambao damu yao inachemka kwenye mishipa yao, wakingojea fursa na kutamani jihad katika njia ya Mwenyezi Mungu.

- Inatia uchungu na kuvunja moyo kwamba jeshi la Jordan, ambalo limetakiwa kujibu kuwasaidia kaka na dada zao huko Gaza, limetulia tuli licha ya kuwa na vifaa vya kutosha na bajeti kubwa ya ulinzi. Dori yake imedunishwa hadi kulinda mipaka ya mashariki kwa ajili ya Mayahudi waoga, na inakanusha haraka vitendo hivi vitukufu vya ushujaa, huku chanzo cha kijeshi kikikanusha haraka kuwa wanajeshi wa Jordan walikuwa wamevuka mpaka wa magharibi!

- Imethibitika kuwa Mayahudi ni watu waoga waliolaaniwa kwa udhalilifu na unyonge. Haijalishi ni kiasi gani tawala zinazoshirikiana nalo zinalinda mipaka yao, kama inavyoonekana wazi, zinajua kwamba mradi wa Ummah ni kuondoa uwepo wao, kinyume na malengo ya watawala wao. Hili linadhihirika kutokana na kauli ya waziri wao wa nishati, ambaye alitangaza kuwa ataharakisha ujenzi wa uzio kwenye mpaka na Jordan.

- Kusitasita kusifia operesheni hii ya kishujaa, kuikana au kutoa kauli za maonyo ya kiuoga kutoka kwa watu wa utawala wa Jordan wakisema, **"Tunaonya dhidi ya kuyumbishwa na mihemko kwa gharama ya usalama na uthabiti wa nchi,"** itarekodiwa kama kushirikiana na maadui wa Ummah na tawala wanazozilinda, zikiwapotosha watu. Hawasimami pamoja na watu wa Jordan, waliokusanyika kwa maelfu kuunga mkono na kupongeza kicha cha kishahidi cha mashujaa wawili wa Jordan.

#### **Wanajeshi wa Jeshi la Jordan... Vizazi vya Maswahaba:**

Vitendo hivi vya kishujaa vya kibinafsi, kukabiliana na adui muoga kwa kuvuka mipaka, na kuuawa kishahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu ili kuyakomboza maeneo matakatifu, Msikiti wa Al-Aqsa, na Palestina yote kutoka kwa Mayahudi na Amerika, ambayo inaendelea kuwapa silaha, vifaa, na ujasusi huku likieneza ufiadini, vinapaswa kuchochea ndani yenu hisia ya heshima na uanaume. Nyinyi watu wenye nguvu mnaoitwa "ndugu wenye silaha" mnapaswa muinuke kumtetea Mwenyezi Mungu, Mtume Wake, na Waislamu, na sio watawala wenu wanaowapeleka kwenye maangamivu na kuwatumikisha kwa maadui zenu. Wallahi, usalama na uthabiti nchini Jordan utakuja pale tu mtakapochukua hatua leo ya kulitokomeza umbile hili ovyo, hivyo kupata radhi za Mwenyezi Mungu na kuandika majina yenu katika kumbukumbu za heshima na adhama.

[وَلَا تَرْكَنُوا إِلَى الَّذِينَ ظَلَمُوا فَتَمَسَّكُمُ النَّارُ وَمَا لَكُم مِّن دُونِ اللَّهِ مِن أَوْلِيَاءٍ ثُمَّ لَا تُنصَرُونَ]

**"Wala msiwategemeo wanao dhulumu, usije ukakuguseni Moto. Wala nyinyi hamna walinzi badala ya Mwenyezi Mungu, wala tena hamtasaidiwa."** [Hud:113]

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Jordan**